**BORESHA VIWANGO**

KAMPENI YA USAWA WA MALIPO YA GREATER PITTSBURGH

# CHUKUA KIAPO

Miji kote Marekani imepiga hatua kubwa katika kuziba pengo la tofauti ya mshahara kati ya wanaume na wanawake. Licha ya kutunukiwa taji la "Jiji Nambari moja la Kuishi", 11 Pittsburgh na maeneo jirani yanaendelea kutatizika kuhusu tofauti ya mshahara kati ya wanaume na wanawake, hasa inapohusu wanawake weusi. Waajiri katika eneo la Greater Pittsburgh wana uwezo wa kuziba pengo la tofauti ya mshahara kati ya wanaume na wanawake.

---

Tunakuomba uboreshe viwango hivi na ujitolee katika kutumia hatua hizi tano muhimu:

**1.** Jitolee kusaidia, kukuza, na kushiriki mapema katika uwazi wa malipo wakati wa mchakato wa kuajiri.

**2.** Hakikisha kuna mchakato wa kuajiri wa haki na usawa kwa kuondoa maswali ya mishahara inayotakiwa na historia ya mishahara katika mchakato wa maombi.

**3.** Toa mafunzo ya kila mwaka ya utofauti wa kampuni ili kushughulikia, kupunguza, na kuelimisha kuhusu upendeleo wa bila kujua na vizuizi husika vinavyoathiri kuajiri, kupandisha vyeo, na utamaduni wa shirika.

**4.** Fanya ukaguzi wa kila mwaka wa tofauti za mishahara ya watu wa jinsia na rangi tofauti miongoni mwa wafanyakazi wanaofanya kazi zinazolingana zinazohitaji viwango sawa vya uwajibikaji, ujuzi, utata na hali ya kazi na kuzingatia viwango vya elimu, uzoefu, wa awali, ujuzi na muda wa kuwa katika kampuni.

**5.** Jitolee kukagua sera na kanuni ili kuhakikisha zinafuata Sheria ya Kitaifa ya Mahusiano ya Kazi ya 1935.

---

Jina, Cheo, Kampuni | Tarehe

**Boresha Viwango ⬆ na Uchukue kiapo cha kuziba pengo la tofauti ya mshahara kati ya wanaume na wanawake!**